HOTUBA YA MHE. BAHAME TOM NYANDUGA, MWENYEKITI WA TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA WAKATI WA HAFLA YA UTOAJI TUZO ZA UMAHIRI WA UANDISHI WA HABARI TANZANIA (EJAT) 2015, UKUMBI WA MLIMANI CITY, DAR ES SALAAM, APRILI 29, 2016

Mhe. Thomas Mihayo, Jaji Mstaafu na Mwenyekiti wa Baraza la Habari Tanzania,
Waheshimiwa Wamiliki wa Vyombo vya Habari,
Ndugu Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania,
Ndugu Watendaji Wakuu na Wahariri wa Vyombo vya Habari,
Ndugu Wawakilishi wa Asasi za Kiraia,
Ndugu Wadau wa vyombo vya habari mliopo hapa,
Ndugu Wanahabari,
Wageni waalikwa,
Mabibi na Mabwana.

Habari za jioni!

Napenda nianze kwa kuushukuru uongozi wa Baraza la Habari Tanzania kwa kunipa heshima ya kuwa Mgeni Rasmi wa siku yenu hii ya leo, itakayoambatana na kuwatambua waandishi wa habari mahiri na kazi zao mbalimbali hapa nchini. Kwa hakika niliupokea mwaliko wenu kwa moyo mkunjufu kwa kutambua heshima mliyonipa mimi binafsi na taasisi ninayoiongoza ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kushiriki kwenye hafla yenu leo. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inatambua michango mbalimbali ya wanahabari na pia umuhimu wa tasnia ya habari kwa ustawi wa taifa letu ikiwa ni mojawapo ya nguzo kuu na muhimu ya uhuru wa mtu kuwa na mawazo na fikra mbalimbali, kuheshimu haki za binadamu na utawala wa sheria.

Nitumie nafasi hii kuwapongeza nyote mliofika mahali hapa. Mmefanya hivi kutokana na sababu moja tu kubwa, kwamba mtambua na kujali umuhimu wa tasnia ya habari ndani ya jamii yetu.

Pia niwashukuru Baraza la Habari Tanzania, kwa jitihada zao kubwa za kuratibu masuala mbalimbali yanayohusu tasnia ya habari na kwa kufanikisha hafla hii - hongereni sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti,
Ndugu Wanahabari, wageni waalikwa,
Mabibi na Mabwana;
Napenda nichukue fursa hii kwa ridhaa yenu, kwa ufupi tu, niitambulishe Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ni taasisi ya kitaifa, iliyoundwa chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kama idara huru ndani ya Serikali, yenye mamlaka ya kusimamia haki za binadamu na utawala bora.

Tume hii ni moja ya Tume nyingi ulimwenguni ambazo zimeundwa kwa kufuata misingi ya Azimio la Baraza Kuu ya Umoja wa Mataifa Na. 48/132 la Desemba 1993 linalotaka nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kuwa na Tume huru. Kwa hiyo Tume hii ni chombo muhimu sana katika taifa lolote linalopenda demokrasia, utawala wa sheria, haki, usawa na amani kwa raia wake wote.

Mamlaka na majukumu ya Tume yameainishwa katika Ibara ya 130(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, pia katika Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391 toleo la mwaka 2002 la sheria za Tanzania.

Kwa uchache tu majukumu ya Tume ni pamoja na: kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini, kama haki hizo na misingi ya utawala bora ilivyoainishwa ndani ya Katiba ya nchi, na mikataba ya kikanda na kimataifa; kupokea na kuchunguza malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, kufanya tafiti na kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora, na kuishauri serikali kuhusu umuhimu wa kuheshimu na kulinda haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Misingi ya utawala bora inayosimamiwa na Tume ni pamoja na umuhimu na ulazima wa kuheshimu utawala wa sheria, (rule of law), uwajibikaji wa Serikali na taasisi za umma, na kila mtu, wakiwemo sekta binafsi, kuheshimu haki za binadamu na misingi ya utawala bora ili kujenga jamii yenye kuheshimu usawa.

Tume imekuwa ikitoa elimu na mafunzo kwa umma kupitia mikutano ya hadhara, semina, vipindi maalum katika radio na luninga, na pia kupitia machapisho mbalimbali.
Napenda nivishukuru vyombo vyote vya habari, magazeti, radio, luninga na mitandao ya kijamii kwa kufikisha elimu hii na taarifa mbalimbali za Tume kwa umma wa Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti,
Ndugu Wanahabari, wageni waalikwa,
Mabibi na Mabwana;
Tume inatambua na kuheshimu mchango wenu katika jamii, na mara kwa mara imekuwa ikisimamia na kutetea uhuru wa vyombo vya habari na taaluma ya uandishi wa habari kwa juhudi zote, ili kuhakikisha haki ya msingi ya uhuru wa maoni, kupata na kueneza habari inalindwa, inatekelezwa na inaheshimiwa kama inavyoelezwa katika Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Kwa mfano, Tume imeshiriki kwa karibu sana katika kupitia na kutoa maoni kuhusu miswada ya Sheria ya Vyombo vya Habari pamoja na Mswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Habari na kuishauri Serikali jinsi ambavyo miswada na sheria husika zinatakiwa kuzingatia matakwa ya Katiba, mikataba mbalimbali ya Kimataifa na kikanda ya haki za binadamu, ambayo nchi yetu imeridhia.

Aidha, Tume imefanya na inaendelea kufuatilia na kufanya uchunguzi wa matukio mbalimbali yanayominya uhuru wa habari na vyombo vya habari nchini na matukio yanayowagusa moja kwa moja wanahabari na kutoa mapendekezo Serikalini kwa utekelezaji.

Ndugu Wanahabari,
Mabibi na Mabwana;
Leo napenda nizungumzie dhana ya uhuru wa maoni, uhuru wa kujieleza, upashanaji habari, na wajibu wa wanahabari. Kwanza kabisa niseme kwamba kwa ujumla uhuru wa binadamu na haki za binadamu, pamoja na mipaka inayowekwa na sheria, ni haki ambazo binadamu anazaliwa nazo. Haki za binadamu hazitolewi na mtu au Serikali. Haki za msingi zinatakiwa kulindwa na kuheshimiwa na kila mtu ikiwemo Serikali. Tasnia ya Habari na Utangazaji ambayo ni kielelezo cha haki ya kuwa na maoni na kupata habari, ni moja ya sekta za huduma za jamii nchini. Tasnia hii inatoa huduma ambayo ni haki ya msingi ya raia kama inavyotamkwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Uhuru wa maoni na kujieleza ni moja ya haki za binadamu ambayo inatambuliwa na Katiba ya nchi yetu ya mwaka 1977 kama ilivyorekebeshwa mwaka 1984.

Ibara ya 18 ya Katiba inasema: "*Kila mtu anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake; anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi; anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake; anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii."*

Tanzania imekubali na kuridhia Maazimio na Mikataba ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika kuhusu haki ya kupokea na kutoa habari. Matamko hayo ni pamoja na Azimio la Ulimwengu la Haki za Binadamu la mwaka 1948, na mikataba ya kimataifa na kikanda.

Ibara ya 19 ya Tamko la Ulimwengu, Ibara ya 19(2) ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa wa mwaka 1966, na Ibara ya 9 ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu, zinatambua uhuru wa maoni na haki ya kutafuta, kupata na kutoa habari, na uhuru wa mawasiliano, haki ambazo kwa ujumla ndiyo msingi wa dhana ya uhuru wa kujieleza na maoni, kwa lugha ya kigeni *"freedom of expression and opinion."* Haki hii, kama zilivyo haki nyingine zote, hutolewa kwa kuzingatia wajibu wa kila raia kwa jamii na uhuru binafsi wa binadamu. Haki au uhuru huu ni msingi mmojawapo, au kigezo kimojawapo cha uwepo wa demokrasia, katika nchi yoyote inayojipambanua kama nchi inayoheshimu demokrasia.

Haki hii imefafanuliwa kupitia maelezo yanayojulikana kama '*General Comment'* Na. 34 ya Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Taifa (United Nations Human Rights Committee).

Katika kikao cha kamati hii kilichofanyika Geneva, Uswisi mnamo tarehe 11 - 29 Julai, 2011, kamati hii ya kimataifa inatamka kwamba uhuru wa maoni na uhuru wa kujieleza ni sehemu muhimu na ya lazima kwa maendeleo ya kila mtu, na jamii. Haki hii ndio jiwe la msingi la kwanza kwa kila jamii huru inayoheshimu demokrasia. Uhuru wa kujieleza na uhuru wa maoni ni haki zinazoshabihiana. Haki hii ni muhimu katika utambuzi wa misingi ya uwazi na uwajibikaji. Maana yake ni nini? Kwa mfano vyombo vya habari visipokuwa huru vitashindwa kueleza habari za uonevu, au za uvunjifu wa misingi ya utawala bora. Vitashindwa kueleza tuhuma mbalimbali za ubadhirifu au za unyanyasaji wa wananchi.

Ndugu Wanahabari,
Mabibi na Mabwana;
Katika kufafanua mkataba huu wa kimataifa Kamati imesisitiza kwamba kila nchi mwanachama inao wajibu wa kulinda na kuheshimu haki hii. Utekelezaji wa haki hii unapaswa kufanywa na mihimili yote ya utawala ambayo ni Serikali, Mahakama na Bunge, na mamlaka nyinginezo zilizopo chini ya mihimili hii.

Kamati imeeleza kwa kina kuhusu haki ya kupata habari (right of access to information). Ili kila mtu aweze kufurahia mkataba huu, kila nchi mwananchama inapaswa kutengeneza taratibu muhimu za utekelezaji wa haki hii. Serikali husika inapaswa kutunga Sheria ya haki ya kupata habari, sheria hii ihakikishe inaweka taratibu za kufuatwa katika upatikanaji wa haki hii kama mkataba unavyoeleza. Kamati pia inazitaka nchi wanachama kuchukua hatua madhubuti za kuhakikisha mtu analindwa dhidi ya vitisho vyenye nia ya kumzuia kupata haki hii. Mfano wanahabari sehemu mbalimbali duniani wamekuwa wakipata vitisho mbalimbali, kukamatwa, kutishiwa maisha, hata kuuawa, Kamati imetoa wito kwa nchi wanachama kukomesha tabia hizo na hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahusika.

Ndugu Wanahabari,
Mabibi na Mabwana;
Pamoja na kuwa Kamati imeeleza misingi ya utekelezaji wa haki ya uhuru wa kutoa maoni, uhuru wa kujieleza na uhuru wa kupata habari, mkataba pia umeweka mipaka (restrictions) kwa wanahabari katika upatikanaji na upashanaji wa habari, endapo habari hizo zinalenga kumchafua mtu au kuchafua jamii, na pia endapo utoaji wa habari utahatarisha usalama wa taifa/nchi. Mipaka hii inapaswa kuainishwa katika sheria zilizotungwa na nchi husika, na itumike pale ambapo ni budi kwa minajili ya ulazima wa kulinda demokrasia.

Ndugu Wanahabari,
Mabibi na Mabwana;
Sherehe hii ni fursa nzuri ya kwa wadau wote, wakiwemo Serikali, wanahabari, wamiliki, taasisi mbalimbali za kiserikali na kiraia kukaa pamoja, kutafakari na kupima maendeleo ya shughuli za tasnia ya habari nchini, uwepo wa uhuru wa maoni na uhuru wa kujieleza na kupata habari, ili kubaini mafanikio na changamoto zilizopo. Lengo kubwa likiwa ni ni kuimarisha mafanikio yaliyopatikana na kutafuta namna ya kukabiliana na changamoto zilizopo mbele yetu. Nchini kwetu sasa hivi tunasikia matukio ya kuminywa kwa uhuru wa kupata habari na kutoa maoni. Waandishi wa habari wamekuwa wakinyanyaswa na hata kutishiwa usalama na maisha yao. Kuna taarifa kwamba baadhi ya waandishi wanaoandika habari zinazowaudhi watu wengine hutishiwa maisha. Vitisho vipo vya aina nyingi. Wapo waandishi waliomwagiwa kemikali za tindikali, wapo waandishi walioshushwa porini na viongozi, wapo waliotishiwa kupotezwa au kutekwa n.k. Wapo wanahabari walioshambuliwa na hata kuuwawa. Haya hayakutokea huko ng'ambo bali yametokea hapa kwetu. Waandishi wa habari kama walivyo raia wengine wana haki ya kuishi na kutegemea kupata ulinzi wa maisha na nafsi zao kutoka kwa taifa na Serikali kama inavyotamkwa katika Ibara za 14, 15 na 16 za Katiba ya nchi.

Mjadala unaonendelea kuhusu kutorushwa moja kwa moja kwa matangazo ya Bunge kunaweza kutafsiriwa kama kuwanyima wananchi haki ya kupata habari kuhusu mwenendo na kazi muhimu inayofanywa wa chombo kikuu cha uwakilishi.

Tasnia ya habari ni muhimu sana katika jamii yoyote ile, kama ambavyo nimeshasema hapo awali. Tume inatambua kuwa vyombo vya habari vina jukumu kubwa na la msingi la kuwapasha wananchi habari, kuelimisha na kuburudisha. Kupitia kwenu wananchi wanapata fursa ya kujua mambo mbalimbali, kuelezea maoni na matumaini yao na hivyo kufikisha ujumbe kwa wanaohusika kwa hatua za utekelezaji.

Kupitia tasnia ya habari Tanzania imekuwa ni moja ya nchi zenye kuonesha mfano mzuri wa kutelekeza dhana ya uhuru wa vyombo vya habari katika bara la Afrika, hata kama bado kuna mapungufu. Hili linadhihirika kutokana na ongezeko kubwa la vyombo vya habari na uhuru wa wanahabari na vyombo vya habari kufanya kazi zenu. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo, hivi sasa Tanzania ina magazeti ya kila siku takriban 13, magazeti yanayotolewa kila wiki 62, majarida 819, vituo vya luninga 27, vituo vya radio 123 vya kitaifa na vilivyo katika jamii, (Community Radio Stations) vilivyoenea nchi nzima mpaka vijijini, na mitandao mingi ya kijamii.

Ndugu Wanahabari,
Mabibi na Mabwana;
Naamini kuwa katika utekelezaji wa majukumu yenu zipo changamoto nyingi sana zinazowarudisha nyuma katika tasnia hii.

Changamoto kubwa na ambayo ni lalamiko la muda mrefu ni ile ya sheria kandamizi dhidi ya tasnia ya habari, hasa baada ya Tanzania kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi. Sekta na tasnia yenu imeendelea **kulalamikia tatizo la** mapungufu ya Sheria ya Magazeti Na.3 ya mwaka 1976 kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria Na. 10 ya mwaka 1994. Sheria hii imekuwa ikilalamikiwa sana kwamba ina mapungufu makubwa, kwa mategemeo kwamba Serikali itasikia kilio chenu. Sheria ya Magazeti (1976) inayataja mambo ambayo kimsingi ni kashfa (defamation), au taarifa za uongo (false statements), ambayo yanaweza kushughulikiwa kama sehemu ya sheria za madai, kuwa makosa ya jinai, kama yalivyo kwenye Sehemu ya VII ya Sheria ya Makosa ya Jinai (The Penal Code Cap 16. R. E. 2002) ambayo hutumika kushtaki makosa kuhusu uhaini na makosa mengine dhidi ya Jamhuri.

Katika Taarifa ya Tume ya Nyalali iliyowasilishwa mwaka 1994 kuhusu mfumo wa chama kimoja au vyama vingi Tanzania, Tume hiyo ilizungumzia Sheria ya Magazeti ikiwa mojawapo ya Sheria 40 kandamizi zilizotakiwa kubadilishwa. Kwa mujibu wa ripoti hiyo sheria hii imempa mamlaka makubwa sana Waziri anayesimamia habari katika maamuzi ambayo yanavunja baadhi ya haki za binadamu na uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa kutoa maoni, kujieleza na kupokea habari (right to be informed).

Kwa mantiki hiyo basi imeonekana sheria hii inakiuka Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini kitu cha ajabu kabisa taasisi zilizoko kwenye tasnia hii, iwe MOAT, MCT, Press Clubs, wanahabari na wanaharakati wanalalamika tu. Hamna yeyote aliyefungua shauri la kikatiba kudai ama sheria au vifungu hivyo vifutwe kwa kupingana na Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977.

Tumeona maamuzi mbalimbali ya Mawaziri yakienda kinyume na uhuru wa habari na kujieleza. Ni gazeti la MwanaHalisi tu ndilo hivi majuzi lililotumia haki yao ya kikatiba kutafuta tafsiri iwapo Waziri alitumia mamlaka yake kwa usahihi au la, na wamepewa haki yao.

Hivi majuzi tumesikia Waziri mwenye dhamana ya habari akitambua mapungufu yaliyomo ndani ya Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976. Tume inampongeza kwa kutamka hadharani kwamba ametambua mapungufu ya Sheria hiyo. Tume inaamini kwamba taarifa hiyo itafuatiwa na mapendekezo ya kutungwa sheria mpya itakayokidhi haja ya kuheshimu uhuru wa maoni, uhuru wa kupata habari na kujieleza kama inavyoainishwa katika Katiba, mikataba ya haki za binadamu ya kikanda na kimataifa. Sasa hivi mjadala unaendelea kuhusu mswada wa Sheria ya Uhuru wa Kupata Habari (Access to Information Act 2015) ulioondolewa Bungeni wakati wa Bunge la 10. Je, utakaporudishwa tena Bungeni utakidhi haja na matakwa ya Ibara ya 18 ya Katiba na mikataba ya kimataifa?

Kuna utata unaoendelea kuhusu jinsi Sheria ya Mawasiliano ya Kieletroniki na ya Posta Na. 3 ya mwaka 2010, au sheria za mitandao zinavyotumika katika kulinda maadili ya kitaifa. Sheria hii pia haiko wazi hasa kuhusu mamlaka sahihi, kati ya Waziri anayehusika na habari na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) mwenye mamlaka ya Kisheria ya kusimamia maudhui (contents), ya magazeti yanayochapishwa kwa njia ya mtandao. Pia kuna malalamiko kuhusu uhalali na matumizi ya sheria za mtandao. Mjadala huo ni kielelezo kwamba haki ya kupata habari na kuwa na maoni katika zama hizi ambapo teknolojia ya habari na mawasiliano inaendelea kukua inaweza kunyimwa au kuminywa, kwa hiyo ni vema Serikali ikaangalia upya ni vipi sheria hizi zinaweza kukidhi mahitaji ya sheria za kimataifa, yaani *"International minimum humana rights standards"* kuhusu haki ya uhuru wa maoni na habari.

Kuna suala la jinsi Shirika la Utangazaji la Taifa linavyoonekana kutumika kama Taasisi ya Serikali na siyo Taasisi ya umma. Azimio la Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu linalosimamia uhuru wa maoni na kupashana habari, linalojulikana kama *The Delaration of Principles on Freedom of Expression* la tarehe 23 Oktoba 2002, linasisitiza umuhimu wa uhuru wa maoni na kupata habari kwa kupitia njia mbalimbali. Azimio hilo linasema pia kwamba vyombo vya habari vinavyoendeshwa na Serikali, vinatakiwa kubadilishwa na kuwa vyombo vya habari vya umma, na kuwajibika kwa Bunge kwa manufaa ya umma na siyo kwa Serikali peke yake. Katika utendaji kazi vyombo hivi vinapaswa kuzingatia misingi ifuatayo:

- Vyombo vya habari vya umma vinapaswa kusimamiwa na Bodi huru ambayo haitaingiliwa kisiasa au kiuchumi,

- Vyombo vya habari vya umma vinapaswa kutengewa fedha ya kutosha ili kuvilinda visiweze kuingiliwa na mamlaka nyingine,

- Vyombo vya habari vya umma vinapaswa kuhakikisha kwamba wigo wa matangazo yake unawafikia wananchi katika maeneo yote ya nchi,

- Huduma inayotolewa na vyombo vya umma lazima ihakikishe kwamba jamii inapata habari za kutosha, habari za kisiasa zenye uwiano sawa hasa wakati wa kipindi cha uchaguzi.

Kwa kuzingatia miongozo na maazimio ya kikanda na kimataifa, Serikali inaweza kabisa kupeleka miswada Bungeni inayokidhi haja za kulinda maslahi ya umma bila kuathiri uhuru wa maoni na uhuru wa kupata habari na kujieleza.

Haya yote ni mambo ambayo ninyi wanahabari, ama kwa kupitia umoja wenu mna wajibu wa kuyasimamia ili uhuru wa wananchi, vyombo vya habari, na wanahabari uendelee kuwepo. Tume itashirikiana na ninyi katika kufaniksha hilo.

Ndugu Wanahabari,
Mabibi na Mabwana;
Changamoto nyingine ni kuporomoka kwa maadili katika tasnia ya habari. Waandishi ni sehemu ya jamii hii ambamo tunashuhudia kila aina ya kuparaganyika kwa maadili ndani ya jamii. Hatukushangaa wakati fulani tulipoambiwa kuwa kuna wizara zilikuwa zinawalipa waandishi wa habari bahasha za *brown* ili taarifa zao ziandikwe vizuri. Sijui kama hilo bado lipo katika zama hizi. Pia kuna hisia kwamba kuna baadhi ya vyombo vya habari 'hutumika' kufanikisha mahitaji rasmi ya makundi mbalimbali, hasa wanasiasa.Wakati wa kipindi cha Uchaguzi nilihudhuria semina iliyoandaliwa na Dar es Salaam Press Club, ambapo wanahabari walilalamikia kwamba wahariri na wanahabari wanaingiliwa na wamiliki katika kuamua nini kiandikwe au kutoandikwa au kuchapishwa!!

Kwa wamiliki kulazimisha kuandikwa habari ambazo ni kinyume na maadili au *editorial policy* ya chombo cha habari ni ukiukwaji wa maadili ya tasnia ya habari. Wanahabari kukubali kutumiwa kwa namna yoyote, huo ni utumwa, maana utakuwa unafanya kazi ya kumtumikia mtu mmoja badala ya jamii inayotegemea taaluma yako kupata habari.

Natoa rai kwa wanahabari wote msikubali kukiuka maadili yenu kwa kupokea rushwa; kama tatizo ni maslahi madogo basi mshirikiane kupaza sauti katika kupigania maslahi yenu, umoja wenu ndio silaha yenu, nasi tunaahidi kuendelea kutetea suala hili katika mamlaka zinazohusika.

Azimio la Tume ya Haki za Binadamu na Watu ya Afrika linasisitiza kuhusu umuhimu wa wanahabari kuzingatia weledi, na kwamba usimamizi wa maadili ya tasnia ya uandishi wa habari unafanyika vizuri zaidi ukifanywa na wanataaluma wenyewe (self regulation). Kwa hiyo ni lazima wanahabari mkakemea kwa nguvu zaidi haya mambo ambayo yanasemekana kushusha weledi ndani ya tasnia yenu.

Vyombo vya habari haviwezi kuonyesha nguvu yake halisi na kuheshimiwa endapo waandishi wa habari hamtashirikiana katika masuala yanayoathiri tasnia yenu. Kwa sasa, kwa mujibu wa takwimu, waandishi wengi ni wasomi wa kiwango kizuri. Wengi wao wanaendelea kuhudhuria mafunzo mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi. Tunatarajia waandishi wazoefu watatumia muda wao kuwasaidia waandishi wachanga katika kuwakuza kitaaluma na kimaadili na kuwaelewesha pale wanapopotoka.

Kwa kuwa mnafanyakazi kwa kuzingatia weledi na maadili ya kazi zenu, basi natoa rai kwenu Waandishi wa habari msivunjike moyo wala kukatishwa tamaa, kwani majukumu mnayotekeleza ni muhimu sana kwa maendeleo endelevu ya taifa letu. Aidha, mtambue kwamba katika utendaji wenu wa kazi ni lazima muwe na ujasiri wa kuhimili vitisho. Ujasiri huu utapatikana kwa nyie kuhakikisha kila siku mnaandika habari zenye ukweli, kwani palipo na ukweli uongo hujitenga.

Kwa kuwa waandishi ni waajiriwa kama waajiriwa wa sehemu au fani nyingine, wanastahili kupata haki zao za msingi kama ilivyo kwa watumishi wengine kulingana na sheria zinazosimamia masuala ya kazi. Kwani kwa mujibu wa sheria za nchi na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, (Ibara ya 23(2), Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu (Kifungu cha 23(3)) na mikataba mingine ya haki za binadamu, kila mtu anayo haki ya kupata ujira wa haki kwa kazi anayoifanya.

Nichukue fursa hii kutoa wito kwa wamiliki wa vyombo vya habari na waajiri wote nchini kuzingatia matakwa ya sheria za nchi na kimataifa kwa kutoa ujira wa haki kwa wafanyakazi wao. Kwa kufanya hivyo watakuwa wanakuza na kuheshimu haki za binadamu nchini. Ni matumaini yangu kuwa wamiliki wa vyombo vya habari watalitizama hili kwa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza la Habari Tanzania,
Ndugu Wanahabari, wageni waalikwa,
Mabibi na Mabwana;
Napenda nimalizie kwa kusema kwamba jukumu la kuifanya tasnia ya habari iheshimike na iwe na mchango wenye tija kwa jamii na taifa kwa ujumla ni jukumu letu sote, yaani mtu mmoja mmoja, tasnia ya habari, jamii, Serikali, asasi za kiraia na sekta binafsi. Lakini wajibu mkubwa bado unabakia kwenu waandishi wa habari, iwapo mtawajibika ipasavyo huku mkizingatia weledi, maadili ya kitaaluma na haki.

Hivyo basi, ni matumaini yangu kuwa zoezi hili la kila mwaka la kutambua michango ya wanahabari mahiri kwa kuwapa tuzo litaendelea kuwa chachu ya kuboresha utendaji kazi katika tasnia hii ya habari. Nichukue nafasi hii kuwapongeza wale wote waliochaguliwa kupokea tuzo hii mwaka huu na miaka iliyotangulia – hongereni sana!

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inawahakikishia kwamba itaendelea kulinda, kukuza na kutetea haki za binadamu nchini, itaendela kupaza sauti na kukemea uvunjwaji wa haki ya uhuru wa maoni, wa kujieleza, na kupata habari, na haki nyinginezo, na pia kuikumbusha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba ina jukumu la kuheshimu uhuru wa vyombo vya habari nchini kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977, na mikataba ya kimataifa na kikanda. Kwa kufanya hivyo, uhuru wa wananchi utaimarika na demokrasia itakua nchini.

Mwisho, nikumbushe kwamba kila penye uhuru na haki, pia kuna wajibu. Vyombo vya habari vina wajibu wa kuhabarisha jamii, kuelimisha na kuburudisha, kwa kuzingatia weledi, maadili, ukweli na kujiepusha na ubabaishaji, upotoshaji na habari zinazoweza kuvunja utangamano wa kitaifa. Vyombo vya habari visitumike kuvunja heshima na utu wa mtu (defamation). Inapotokea ni budi vyombo hivyo vikaonyesha weledi na uwajibikaji.

Napenda nirudie kuwashukuru Baraza la Habari kwa kunialika kwenye hafla hii – asante sana!

Asanteni sana kwa kunisikiliza.